# JUMANNE KATIKA MSITU WA MAAJABU

‘Ina kisengerenyuma’

Hakimiliki © Mwanawetu Mmuni
Mwanawetu Mmuni
P. O Box 90,
Mtwara, **TANZANIA**
Simu: +255 737966996

Chapa ya kwanza 2017
Lulu Self-Publisher
eBook
Mtandaoni: ISBN 978-1-387-01363-0

**© 2021**

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kufasiri, kuchapa, au kutoa kitabu hiki kwa njia yeyote ile bila idhini ya Mwandishi

VITABU VYA MWANAWETU MMUNI TANGU 2017

1. Hasira ni hasara
2. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 1
3. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 2
4. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 3
5. A life after Beijing
6. **Jumanne katika msitu wa maajabu**
7. Kilimo chetu: Karibu sherehe za Nanenane ki-taifa Lindi 2017
8. Come with me
9. Dharau
10. Imani yangu
11. Ken na Kandi
12. Jifikirie
13. NIFIKIRIE; hii ni hali
14. Nadharia ya maisha ya mti na mtu
15. Falsafa Mtandaoni
16. Safari ya Mikumi
17. Mwenge wa Uhuru na Ukombozi wa Fikra
18. Mzigo wa jirani
19. Unamjua huyu?
20. Hadithi za karne ya 21
21. Elimu mtaani
22. Chumbani
23. Umebadilika
24. Kiburi chaponza kichwa

# YALIYOMO

UTANGULIZI ..... 5
SAFARI YA KIJIJINI ..... 6
SAKA MIMBA ..... 17
TUMBO LA MSITU ..... 21
MWENYE KISU KIKALI…! ..... 23
Msituni ..... 29
Kuvunja miiko ya msitu ..... 33
DARAJA LA MTI MMOJA ..... 35
MIZIMU ..... 42
SIMBA MWENYE MJI ‘NAKANJI’ ..... 42
Usiombe ya kukute ..... 45
KIMOMBO ..... 49

# UTANGULIZI

Tamthiliya hii inahusu utamaduni wa jamii ya watu wanaoishi katika msitu wa Mtonyange ambao ni miongoni mwa hifadhi ndogo za pori tengefu la Selous Mkoani Lindi.

Ndani ya msitu huo kuna maajabu mbalimbali ikiwemo binadamu kuheshimu wanyama pori kama vile Simba na Kiboko katika ulinzi wa maisha yao ya kila siku. Simba huyo wanamwita Nakanji na Kiboko anajulikana kwa jina la Kimombo.

Je, simba ataweza kulinda binadamu?

 © 2021

# SAFARI YA KIJIJINI

Jumanne na Cathbet walikuwa ni wanafunzi wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya juu ya Kibiti. Wazazi wa Cathbet waliishi mkoani Mbeya wakati wa Jumanne waliishi jijini Dar-es-salaam. Urafiki wa wanafunzi hawa ulikaribia undugu wa damu kwa kuwa ulifahamika na wazazi wote wa vijana hao. Watu wasiofahamu historia ya maisha yao walidhani ni ndugu wa familia moja. Hata baadhi ya walimu wao walijua walipelekwa katika shule hiyo makusudi.

Likizo kubwa yenye msimu wa mvua ilipofika, wanafunzi hao waliamua kwenda kijijini Chepechepe alikoishi bibi yake Jumanne. Kijiji hicho kipo kwenye hifadhi ya taifa ya pori tengefu la Selous. Mpango wao ulibarikiwa na wazazi wao sambamba na kuwapa nauli.

**MAMA JUMANNE**; Mnakokwenda ni kijijini sio vizuri mkaenda kumsumbua bibi yenu kutaka vitu vya mjini. Mara ooh hiki sili, mara kile nina 'allergy'….! Kama mnajijua ninyi ni watoto wa mjini, kaeni hapa hapa msome 'tuition'. "*Alizungumza hayo wakiwa wapo sebuleni anakabidhi nauli iliyotolewa na baba Jumanne kwa ajili ya safari na fedha kidogo ya matumizi.*"

Jumanne na Cathbet walitabasamu wakifurahia kukubaliwa mpango wao wa safari wakati huo walikuwa

wamekaa kwenye moja ya masofa mazuri ya ngozi yaliyomo sebuleni.

**JUMANNE**; Asante mama, tunashukuru kwa kuibariki safari yetu. Ninakuahidi kutomsumbua bibi wala mtu mwingine yeyote. Hivi baba yuko wapi? Bado hajarudi toka kazini?

**MAMA JUMANNE**; Alirudi, lakini ametoka tena.

**CATHBET**; Asante mama ubarikiwe. Natumaini hatutakuangusha! Mimi nimezoea kuishi kijijini. Kabla ya kufariki babu na bibi yangu, walikuwa wanaishi Mbozi vijijini. Sijui mjamaa hapa? *"Alimwangalia Jumanne akitabasamu"* …..Lakini ninafikiri ataweza ingawa sikufahamu.

*Wazo la kwenda kwa bibi yake Jumanne lilitolewa na Cathbet.*

**MAMA JUMANNE**; Sawa! Vipi mlishaandaa mabegi? Mnatakiwa kurauka ili muwahi kufika njia panda mapema. Sitaki ujinga uko….! Mabinti wa watu na wake za watu, marufuku! Nimeshatuma kachero wakuwafuatilia. Kwa sababu ninajua watakapowaona watoto wa mjini mmefika pale mkiwa mmenona, watadhani mambo safi kumbe nanyi ni kula kulala. Mtampa aibu baba yenu aje kushindwa kwenda kumsalimu mama yake na ndugu zake wengine kutokana na aibu mtakayoitengeneza. Nawatakia

 © 2021

kila la heri katika safari yenu. Mtapelekwa na baba yenu asubuhi ili awatafutie gari yenye safari ya uhakika.

**JUMANNE** na **CATHBET**; Asante sana mama. Usiku mwema nawe pia.

**JUMANNE**; Tutazingatia uliyotushauri.

*Waliingia vyumbani kulala;*

Jumanne na mwenzake waliendelea kuweka vitu vyao vizuri katika mabegi yao hadi walipoamua kujiridhisha vinatosha. Walibadilisha nguo hizi na zile wakizijaribu na kuzivua.

**JUMANNE**; Hapa vipi? “Alimuuliza Cathbet.”

**CATHBET**; Hapo sawa! “Alijibu na kuweka dole ya mikono miwili kwa msisitizo”.

Jumanne alivaa bombo yenye kuvuka magoti, shati dogo lenye kuonesha mkanda na endapo ikimlazimu kuinama nguo za ndani pamoja na kiuno vitaonekana hadharani. Pia miguuni alivaa raba pamoja na stokingi za pundamilia halafu kichwani alipachika kofia yenye ncha wakati mkononi alishika simu janja kubwa yenye ufa aliyopewa na mama yake baada ya kupata hitilafu hiyo.

**CATHBET**; Umependeza mwana lakini kimjini mjini, kijijini noma. Unakumbuka mama alivyosema?

**JUMANNE**; Acha ubabu babu wewe! Kwani tunakwenda nae? Haya ndiyo mapigo we baki na suruari zako za….!

**CATHBET**; Ooh! Chukua. Lakini usichukue pamba nyingi za mtindo huo.

**JUMANNE**; Poa. Naomba hii fedha uweke wewe *"Alimkabidhi kititi cha noti*" ….tutakwenda kujua cha kufanyia tukifika. Pia hata zawadi za bibi naomba ziweke kwenye begi lako, la kwangu limejaa sana halina nafasi tena.

**CATHBET**; umechukua nguo nyingi sana, kama unahama? Poa lete niweke humu.

Mama Jumanne hakutaka safari ya mwanawe ya kwenda kijijini na walibishana sana na mumewe kuhusu kutoa ruhusa. Alihofia; mazingira, vyakula, pamoja na marafiki wa kishamba kwa mtoto wake. Alifikiria watakutana na wasichana wa kijijini ambao ni maskini na kupendana nao. Lakini mwenye kwao 'baba' alitoa ruhusa na kufurahi sana alipomsikia mwanaye anakumbuka kwenda kuzuru kwa mama yake. Alimpa Jumanne zawadi nyingi za kumpelekea bibi yake bila mkewe kujua.

Jumanne akiwa safarini basi linachanja mbuga, ameketi kwenye kiti cha pembeni anachungulia nje kupitia dirishani mawazo tele kichwani. Alikumbuka;

**BABA JUMANNE**; Hakikisha mama yako havioni vitu hivi. Nenda kavifiche chumbani kwako.

**JUMANNE**; Kulikoni mbona kwa siri?

**BABA JUMANNE**; Fanya kama nilivyokuambia sihitaji maswali. *Wanawake wa mjini wanajifanya hawajui kama tulizaliwa kijijini walipotuona mjini tumeulamba mkanda nje.*

Baba Jumanne aliongea maneno hayo kama mtu anayeongea peke yake sababu hakuhitaji ushirikiano na mwenzake. Alishika kifua na kuanza kupangusa shati lake karibu na mfuko kwa viganja cha mkono kana kwamba limenasia kitu au uchafu.

**JUMANNE**; Sawa baba nitafanya hivyo.

Makabidhiano yalifanyika kwenye maegesho ya magari ndani ya uzio wa nyumba yao ya kifahari aliporudi toka kazini muda wa chakula cha mchana. Wakati huo Mama Jumanne hakuwepo nyumbani na baada ya tukio hilo alirudi tena ofisini.

**JUMANNE;** “Alijisemea moyoni” …..Sijui mama hampendi bibi? Aah! Shauri yao wenyewe! Mambo ya kike hayo.

Aligutushwa mawazoni walipofika Nangurukuru hotelini kwa ajili ya kupata chakula na *kuchimba dawa*. Walinunua “take away” na kurejea garini na safari iliendelea.

Walifika njia panda paitwapo Kilanjelanje na kuteremka kwenye basi kubwa liitwalo Maning nice lililokuwa linaelekea Mbinga kupitia Lindi-Masasi-Songea hadi

Mbinga. Basi liliendelea na safari na kuwaacha vijana hao wakisubiri Noah zinazoelekea kijiji cha Nanjilinji.

Safari ilianza kuwa ya karaha pale walipoingia katika daladala ambayo abiria hukaa kwa kupakatana na wengine kuwekwa kwenye buti la gari hiyo.

Mnamo saa kumi na moja jioni waliwasiri kijiji anachoishi bibi yao na kumkuta anawasubiri barabarani.

**BIBI**; Karibu mume wangu…!

Jumanne aligundua huyo ndiye bibi yake kupitia kauli hiyo kwasababu walikuwa hawajaonana kwa muda mrefu hivyo hakuwa na kumbukumbu ya sura yake. Mara nyingi bibi alipokuwa anakwenda jijini Dar-es-salaam kusalimia, Jumanne huwa shuleni.

**JUMANNE**; Asante mke wangu. Leo nimekufuata huku huku na mshenga ili nimalize kabisa. Sitaki utani mie! “Alimshika mabegani, mizigo ikiwa chini.”

Kicheko!

**BIBI**; Leo mimi mbona ni mwanamke kweli kweli sijui nikubebe? Katika mazuri aliyoyafanya Liganga (baba yake Jumanne) ni pamoja na kuniletea mpenzi wangu aah…! “Alipiga makofi” ….Mmh! Karibuni sana. Karibu shemeji yangu.

Bibi alimpokea mfuko mdogo wenye chupa za maji safi ya kunywa yanayotengenezwa na kampuni ya Kitanzania ya Kilimanjaro.

Jumanne alikumbuka kitu na kuanza kukariri maneno ya bibi yake;

**JUMANNE**; "*Alichofanya Liganga chenye kufurahisha"* na kuendelea kukumbuka;

**BABA JUMANNE**; Waache waende…! Nitawapa nauli kama watashindwa, watarudi hata kama itakuwa ni siku ya pili.

Siku ambayo walitoa wazo la kusafiri wakati wakiwa mezani wanamalizia kula chakula cha usiku. Mama Jumanne alicharuka na kutaka kuanza kuzuia safari.

**MAMA JUMANNE**; Unakujua? Unadhani kwa mchezo? Ni mbali hauwezi.

Hivyo Jumanne aligundua furaha ya baba yake juu ya safari yao. Hawakukawia kufika nyumbani sababu hapakuwa mbali kutoka barabarani hadi kwenye kibanda anachoishi bibi yao. Mizigo walisaidiwa kubebewa na wanakijiji waliokwenda stendi kuwashangaa watanashati walioteremka garini. Zilisikika sauti;

**SAUTI**; "Ukisikia mashalobaro ndiyo hawa. Wewe hatari ninachokuambia…!"

**MAMA RUKIA**; Mama Sada! Mama Sada! Njoo tumsaidie Binti Mwema kubeba mizigo ya wageni wake.

**MAMA SADA**; Kwe! Bibi wewe! Wenyewe wapo wapi?

Alionesha mwelekeo bila kuongea ingawa walishakuwa wamezuiwa na ukuta wa nyumba iliyombele ya nyumba wanayokwenda.

**MAMA SADA**; Ooh! Wenyewe ni wale mashaloo?
**MAMA RUKIA**; Bibi wewe watakusikia. Wenyewe huyu ooh!
**MAMA SADA**; *Inadopa* hiyo!
**MAMA RUKIA**; Vya mjini, Sijui nini? Leo Mwema atafaidi kweli….! Usiku lazima nimtembelee.
**MAMA SADA**; Bibi wewe unaanza. Mumeo atakuwa kaenda wapi?
**MAMA RUKIA**; Aah! Kipo kwanza? Nitamtoroka.

*Kicheko na kugongeana mikono.*

Walijikuta wameshafika kwenye nyumba ya bibi yake Jumanne na kuwakuta watoto wamejaa pembeni ya uwanja wa nyumba hiyo.

**MTOTO 1**; Wasanii tunaowaona kwenye video ndiyo hawa.

**MTOTO 2**; Mmh! unadanganya. "Aliongea mtoto mwingine wa makamo."

 © 2021

**MAMA SADA**; Ninyi watoto nendeni kwanza nyumbani mtakuja kuwasalimia kesho, leo wamechoka. "*alisengenya*" ……Binti K wala kuwapangusa sura watoto hawa! Angalia walivyokuwa na matongotongo. '*Aliongea kwa mnong'ono ili wageni wasisikie."*

Mama Sada na mwenzake walipofika nyumbani kwa bibi yake Jumanne, waliingia moja kwa moja ndani ili kwenda kutua mizigo halafu walirudi nje na kuketi barazani walipokaa wageni. Jumanne na Cathbet walikuwa wamekalia viti vya mbao *mkao wa nyani* ndipo mabinti hao walipowasogelea na kukalia miguu yao.

**MAMA RUKIA**; Habari za safari wageni.
**CATHBET**; Salama, wazima?
**WOTE**; Njema, sijui nyinyi?
**MAMA RUKIA**; Mmesafiri salama?
**CATHBET**; Safari ilikuwa poa. Karibuni.
**WOTE**; Karibuni ninyi wageni. "*Walijibu wakiangaliana kama wanashangaa kukaribishwa."*
**CATHBET**; Asanteni.
**MAMA SADA**; Habari nyingine? "Alimuangalia Jumanne ambaye hakujibu ilionesha hakuelewa kama anasalimiwa hadi aliposhtuliwa na Cathbet kwa kumtingisha.
**JUMANNE**; 'What'?
**CATHBET**; Wanakupa 'hi!' *Mashori*
**JUMANNE**; (Alitabasamu) Poa. Unajua uchovu, poleni nilijua bado mnamalizana na 'brother' hapa.

**WOTE**; (Walicheka) Pole wewe! Karibu sana.

*Alitokea Bibi yake Jumanne (Mama Liganga au binti Mwema) toka ndani na kuingilia mazungumzo yao.*

**BIBI**; Kwani bibi wewe mumeo yupo nyumbani? "Alimuuliza Mama Sada"

**MAMA SADA**; Hayupo amekwenda kijijini Mbuyuni kuchukua mbegu ya ufuta. Vipi unamhitaji?

**BIBI**; Nilitaka aniunganishie 'solar' yangu, giza limeshaingia.

**JUMANNE**; Yaani mumeo nipo hapa, bado unahitaji msaada kwa majirani? Mwanamke wewe! Ngoja nifanye mambo nikuoneshe baba mwenye nyumba kaja.

*Wote walicheka.*

*Bibi, Cathbet na Jumanne Waliingia ndani kuwasha taa wakati wanawake hao wawili waliaga na kuondoka.*

***

Kilichomfikirisha Jumanne hadi kutosikia salamu ni mazingira na hali ya maisha ya bibi yake kwa ujumla. Moyoni alijilaumu kwenda na rafiki yake kwa madai ya kuona aibu. Jumba waliloamka siku hiyo la mtoto wa ajuza huyo ni la kifahari. Hakuweza kuamini kama Mama Liganga anaishi katika kibanda kidogo *mbavu za mbwa* kilichoezekwa kwa mabati mepesi, kuta za miti zilizochapiwa kwa kutupiwa tope kwa mkono na ndani kulikuwa na sakafu ya udongo badala ya saruji. Ndipo Jumanne alipopatwa na simanzi moyoni.

**JUMANNE**; Au mama yangu ndiye kikwazo? Huenda anamzuia baba kuja kumjengea nyumba imara mama yake. “Aliwaza.”

Baada ya kuoga kwenye msala uliozibwa kwa kutumia makuti ya miti ya mivumo ulionekana kuwa mpya labda ulitengenezwa baada ya taarifa za ujio wa wageni. Sakafu ya msala huo ilikuwa imepangwa magogo ya miti. Jumanne alishangaa sana usanifu wa jengo hilo.

Wakiwa wanakula chakula cha usiku;

**CATHBET**; Chakula ni kitamu sana shemeji. Naona kaka amefurahi sana.

**BIBI**; Kama hasingelikuja, nilipanga Jogoo huyu nimpeleke huko huko mjini ili amle likizo ijayo.

**JUMANNE**; Ewa wee! Mambo si ndiyo hayo! Raha ya mke bora akufikirie hata kama ukiwa mbali nae. Asante mke wangu.
*Kicheko*.
Baada ya utambulisho wa mgeni waliagana na kuoneshwa chumba chao cha kulala. Ndani ya chumba kulikuwa na vitanda viwili, kimoja cha mbao na kingine cha kamba wenyeji huita *teremka tukaze*. Ilionesha bibi yake Jumanne alikihama chumba chake kupisha ugeni.

## SAKA MIMBA

*Usiku ngoma zilisikika barabara!*

Jumanne uzalendo ulimshinda na kumuamsha bibi yake kwa kupaza sauti angali chumbani. Ilikuwa rahisi kwao kuwasiliana kwa kuwa nyumba hiyo haikuwa na dari. Aliuliza;

**JUMANNE**; Ngoma hiyo ni ya nini?
**BIBI**; Vijana hao, wameshiba dona kwa mbaazi.
**JUMANNE**; Una maanisha nini?
**BIBI**; Hakuna shughuli yeyote bali ni burudani kwa vijana ingawa siku hizi haina mvuto sana. Ngoma hiyo inafana nyakati za msimu wa mavuno ambapo watu wengi huwa na fedha baada ya kuuza ufuta na kufanya shughuli za kuwacheza watoto unyago. Hiyo ni *saka mimba* na muda si mrefu watazima ngoma. Vipi mnataka kwenda kuiona? “Aliuliza aliposikia sauti ya Cathbet akimnong’oneza jambo Jumanne.”
*Waliangaliana na kukonyezana*.

**JUMANNE**; Mmh! Hakuna simba? Maana ni nje huko. “Aliuliza swali lenye kutilia shaka mazingira wakati alionesha dhahiri shahiri kutaka kwenda ngomani.”

**BIBI**; Kama hamjachoka, twendeni niwapeleke nyumbani kwa Baba Sada ili muambatane nae. Yeye ni kijana mwema na jasiri.

Kauli ya bibi yake ilimtoka Jumanne chumbani kwa haraka alimanusura ajigonge kiwambaza shati kalishika mkononi.

**JUMANNE**; Sawa mama watoto. Twende nikaone halafu nitarudi sasa hivi, sitakawia.
**BIBI**; Mwenzako haendi?
**JUMANNE**; Tunakwenda sote, lakini haujajibu kuhusu simba.
**BIBI**; Hamna simba. Nendeni lakini msichelewe kurudi na wala msikae kipembeni peke yenu.
**JUMANNE**; Sawa mama umesomeka. "*Alimshika mkono na kuutikisa taratibu kisha kuendelea kuushika wakiambatana kutoka nje wakifuatwa na Cathbet.*"

Ilishatimu saa tatu ya usiku. Ngomani waliwakuta watu wengi, wake kwa waume na wakubwa kwa wadogo. Wasichana vigoli mwali walicheka cheka ovyo. Wapo waliokaa na wengine walisimama pembeni ya uwanja. Katikati ya duara kulikuwa na moto mkali wa kuni unaowaka na kufanya wadudu kuruka ruka juu angani. Walikaribishwa na mshangao na sauti za chini zisizosikika vizuri lakini zilihusiana na sifa za muonekano wao nadhifu.

**MSICHANA 1**; Nenda…! "Alimsukuma mwenzake kuelekea waliposimama akina Jumanne."

**MSICHANA 2**; Nani? Ugonjwa! Wamjini hawa hawachelewi kukupigisha mswaki.

Kicheko!

**SAUTI**; Ninyi keleleni watawasikia. Endapo wakimpenda mtu miongoni mwetu, watamchagua.

**SAUTI NYINGINE**; Na kweli…! Wanakuchukua video hao, sasa ninyi wenye miguu yenye nyufa si mtawatisha watazamaji?

**SAUTI**; Mmh woga tu, hamna lolote.

Ngoma iliendelea kupigwa kwa kasi. Akina dada na vijana wa kiume walikuwa wakishindana kumwaga machezo na kuzungusha viuno mithili ya feni. Mwanga wa moto ulionesha waziwazi mavazi yao. Vijana wengi waliojiona wakileo walivaa nguo zenye rangi angavu, na mikufu. Kwa upande wa wanawake waliviringisha shanga nyingi shingoni sambamba na bangili nyingi mikononi na heleni zenye rangi mbalimbali masikioni.

Vijana wanaojiona *mababu-kubwa* wa kijijini walianza kuwa vikundi vikundi huku *wakiwazengea* kuashiria wanateta jambo juu yao. Cathbet aliugundua mchezo na kumuomba Jumanne na Baba Sada warudi nyumbani. **CATHBET**; Ninahitaji kulala, ninahisi usingizi umejaa

machoni. Unakumbuka bibi alisema, “tusichelewe?” Halafu tunamchelewesha kulala na yeye pia kwa kutusubiri turejee ili atufungulie mlango.

Jumanne aliposikia kuhusu bibi yake, alikubali kurudi nyumbani *kishingo upande*. Nyumbani walimkuta bibi yao kakaa karibu na jiko anawasubiri akiwa anasuka ukili.
**CATHBET**; Kumbe haujalala? Poa ‘brother’ kesho tutazungumza. “Alimuaga Baba Sada.”
**BABA SADA**; Hakuna noma, alamsiki. “Aliondoka.”
**BIBI**; Nilikuwa ninawasubiri. Vipi ngoma mmeifurahia?
**JUMANNE**; Sana tu! Ilibaki kidogo na mimi nimchague wa kwangu.
*Walicheka!*
**BIBI**; Kama ndivyo basi nashukuru lakini hayo machaguo yako mapya yangezua ugomvi
**JUMANNE**; Wewe ndiye wa ukweli. Jiamini hayupo wakukunyang’anya tonge mdomoni. Fikiria kidume hadi nimekufuata huku!
*Walicheka.*
Walifunga mlango wao na kwenda kulala. Usiku baada ya kuzimwa ngoma zilisikika sauti mbalimbali za wanyama.

 © 2021

## TUMBO LA MSITU

Asubuhi walisikia sauti mbalimbali za ndege na baada ya kutoka nje waliwaona makundi kwa makundi wakiruka na kutoa mvumo kama mshindo wa kitu kinaanguka, “uwuuuh!”

**CATHBET**; Kitoweo hicho *mwana*.
**JUMANNE**; Duh! Ni wengi sana sijui wanaishi wapi?
**CATHBET**; Ulisikia sauti ya fisi usiku?
**JUMANNE**; Fisi?
**CATHBET**; Ndiyo….! Tena na wanyama wengine wengi lakini sijui ni ya wanyama gani. Nilikumbuka tulikuwa nje masaa machache, nikajua kwanini bibi hakulala hadi tuliporudi.

Jumanne aliduwaa akiwa kashikilia mswaki mkononi huku kaegemea mti wa muhogo uliostawi vizuri nyuma ya nyumba ya bibi yake.
**JUMANNE**; Kweli? Sema unatania…!
**CATHBET**; Nani akutanie? Muulize bibi. Kuanzia leo naingia na kopo la kukojolea mkojo ndani. Sitoki tena nje usiku ng’o!
**JUMANNE**; Sasa tufanye hivi, leo usiku uniamshe endapo utasikia tena sauti za wanyama. Tuachane na habari za bibi.
**CATHBET**; Poa.

Baada ya kupata staftahi walikwenda kuteka maji mtoni wakiambatana na vijana wenzao. Walikutana na msitu mnene wenye kusisimsha vinyweleo. Jumanne na Cathbet hawakutaka kubakia nyuma wala kuwa mbele. Walibaki kati ya msafara kuanzia mwanzo hadi mwisho wa safari. Walitumbua macho kama vile mjusi aliyebanwa na mlango. Walistaajabu zaidi pindi walipofika mtoni na kukuta maji yana rangi ya hudhurungi. Rangi hiyo ilisababishwa na majani mengi makavu ya mitomondo kudondokea kwenye mto.

Pia kulikuwa na nyayo za wanyama mbalimbali. Walipofanikiwa kurudi nyumbani salama waliomba kuelekezwa sehemu nyingine ya kuteka maji hata kama ni mbali. Ndipo walipoelekezwa kwenye kisima cha pampu kilichopo kwenye kijiji cha pili ingawa ni mbali ukilinganisha na mtoni. Lakini waliona heri ya umbali kuliko taharuki ya mtoni na kuchagua kuchota maji kisimani.

Bibi aliwafurahia wajukuu zake kwa sababu hawakuwa wakorofi na walimsaidia kazi mbalimbali kama vile; kuchota maji, kuosha vyombo, kulima na waliweza kufagia kwa kutumia fagio ya nyasi. Walishindwa kupika sababu ya aina ya nishati iliyotumika kupikia ambayo ni kuni.

***

 © 2021

**MWENYE KISU KIKALI…!**

Siku moja asubuhi Cathbet akiwa anaendelea kushughulika na masuala ya usafi alikuwa amevaa kaptura yenye kuacha nje eneo kubwa la miguu yake, mara ghafla bibi alitokea.

**CATHBET**; Shikamo bibi! Umeamka salama? *"Aliinuka na kusimama wima na kuanza kuchezea ufagio kwa kuchomeka vizuri vijiti vya fagio kana kwamba vilikuwa vimekaa shaghalabaghala."*

**BIBI**; Marahaba! Mimi ni mzima sijui wewe.

**CATHBET**; Niko poa shemeji yangu. Naomba uende ukapumzike tu, usafi na mambo mengine niachie mimi.

**BIBI**; Hicho ndicho ninachokupendea shemeji yangu, huna makuu. Mbona nimeshaanza kupata mwili mie…!

**CATHBET**; Na bado…!

*Kicheko! Mara Jumanne alitokea;*

**JUMANNE**; Mnafurahi tu wenyewe. "*Alijinyoosha na kupiga mwayo mrefu huku anafikicha macho kuonesha bado ana usingizi*." …..Shikamo bibi!

**BIBI**; Marahaba mjukuu wangu! Furaha lazima. Hivi kweli ninavijana barubaru watu wa zama hizi wanawaita "wa ukweli" ninaanzaje kununa? Wanawali hawaishi kunisaidia kufanyakazi zangu. Ingawa ninawivu mie…!

Kumbukumbu: Kuna siku wasichana wawili walikuja kuleta ndoo za maji walizokwenda nazo kisimani vijana hao na wenyewe walibakia kijiweni na kumkuta bibi anapika.

**SAUTI**: Hodi..!

 © 2021

**BIBI**; Karibuni! Ooh! Mwanakheri…! Karibu…..karibuni.
*Wanawali hao walipeleka ndoo za maji ndani kisha kutoka nje kusalimiana na mwenyeji wao.*
**MWANAKHERI**; Asante bibi, Shikamo!
**HIDAYA**; Shikamo bibi!

Walikuwa na nyuso zenye soni huku wakitembea kwa kuburuza vidole na kuigonganisha miguu kama wanacheza manganja. Pia walizaba sura zao kwa kanga zilizovingirishwa.

**BIBI**; "*Aligundua jambo lakini aliamua kuzuga na kujifanya hajaelewa chochote na aliuliza,*"….mmewaacha wapi kaka zenu? Halafu ninapika na nilishawaambia wasichelewe.
**HIDAYA**; Tumewaacha wanasalimia wenzao kijiweni. Sisi tulipita njia ya nyuma.
**MWANAKHERI**; Nasikia sauti zao watakuwa wanakuja.
**BIBI**; Bora! Nawashukuru wajukuu zangu, maana bila ninyi nadhani hata maji yangelichelewa hivyo hivyo. Vipi nyumbani, kwema? Hidaya baba yako hajarudi porini? Maana mboga inapatikana kwa shida sana na wageni kuwalisha mlenda kila siku au….?
*Walicheka!*
**HIDAYA**; Amerudi lakini hakupata windo kubwa. Alipata paa mmoja tu na tayari amenunuliwa. Labda akienda tena kesho, nitawahi kukujulisha mapema.
**BIBI**; Sawa. Karibuni kula, chakula kimeshaiva.
**WOTE**; Asante bibi kwa kutukaribisha. Waandalie tu wageni sisi tumeshiba.

**BIBI**; Nanyi pia ni wageni wangu halafu mmefanyakazi ngumu ya kuchota maji.
**WOTE**; Asante, kwaheri.
**MWANAKHERI**; Haya tunakwenda.
**BIBI**; Ndiyo hamsubiri chakula?
**WOTE**; Asante, tutakula siku nyingine.
*Waliondoka*.
Cathbet na Jumanne walicheka na kugongesha mikono baada ya kukumbushwa jambo hilo.

***

*Cathbet alivuta kumbukumbu ya tukio lilivyokuwa. Wakiwa njiani hawana hili wala lile ghafla walikutana na Hidaya pamoja na Mwanakheri kisha mambo yakawa hivi;*

**HIDAYA**; Ninyi mnapenda maji kama vyura? Muda wote mna ndoo vichwani…!
*Aliongea akiwa anatabasamu na kumsalimia Cathbet kwa kumpa mkono.*
**JUMANNE**; Salamu kwanza warembo! Mambo ya kuchaniana mkeka yanatokea wapi?
**MWANAKHERI**; Ukiona hivyo mjue mmezidi….! "*Aliongea kwa madaha na kumpokonya ndoo Jumanne."*
**JUMANNE**; Afadhali leo mtusaidie nyura sie!
**MWANAKHERI**; Yamekuwa hayo?
**CATHBET**; Mmh! *"*Alimuelekezea Hidaya ndoo yake ili aichukue."
**HIDAYA**; Lakini…..! *"Alibana midomo na kumtingisha kichwa kwa kumsukuma kwa kidole alichokitua taratibu juu*

*ya paji la uso wa Cathbet kisha alichukua ndoo na kuendelea kuongea,"* haya tutafanyaje na tumelikoroga acha tulinywe.
**JUMANNE**; Mambo si ndiyo hayo? Warembo kama ninyi hampaswi kuwa wakatili na roho mbaya. *"Alimuangalia Cathbet na kumkonyeza."*

Waliamua kuacha kutumia barabara kuu inayoelekea kisimani na kupita njia ya kichochoroni. Walipokuwa wanatembea, walitumia muda huo kucheza na kushikana shikana hadi walipofika kisimani kisha kuchota maji na kurudi nyumbani.

**JUMANNE**; MWANA, kesho nitakutafuta tupange tukae wapi tuongee ili unipe michapo ya hapa kijijini. Sawa?
**MWANAKHERI**; Michapo yote hii haujaridhika hadi ya kupanga?
**JUMANNE**; Acha ujinga! *"Alimpiga kofi dogo begani na kuendelea kujieleza,"* ndiyo hivyo! Kesho mchana utaniona napita maeneo ya nyumbani kwenu, dakika chache zikipita unifuate. Sawa mama?
**MWANAKHERI**; Aah! Unanishtua. Nikimwaga maji ujue sirudi tena kuchota mengine bali utakwenda peke yako. Sawa nitakufuata. *"Alijibu akijichekesha."*

*Wakiwa nyuma nyuma wawili hawa waliongea kwa usiri mkubwa.*
**CATHBET**; Kama vile mama.
**HIDAYA**; Poa.

 © 2021

Hidaya na Cathbet walionekana kama vile yao yalishaeleweka na tayari walishayamaliza lakini ilibaki kuwa siri ya mtungi. Waliwaficha wenzao kuhofia kuleta umajununi na kusababisha kumwaga mchele kwenye kuku wengi.

**JUMANNE**; Tunatoa 'hi!' kijiweni mara moja hivyo ninyi tangulieni.

Cathbet na Jumanne walielekea kijiweni wakati Hidaya pamoja na Mwanakheri walilazimika kufikisha maji nyumbani.

***

*Baada yakutoka mawazoni, Cathbet alikumbuka jambo;*

**CATHBET**; Jumanne, unakumbuka leo ndiyo siku tuliyopanga na wale jamaa kuwa tutakwenda kuvua samaki?

**JUMANNE**; Aah… kumbe ni leo?

**BIBI**; Wapiii?

JUMANNE; Nanganyamwa.

**BIBI**; Kufanyaje?

**CATHBET**; Vipi bibi?

**BIBI**; Hamtaweza.

**CATHBET**; Ni mbali sana?

**BIBI**; Sio mbali sana lakini msituni kuna mambo mengi na ninyi hamjazoea pilikapilika za porini. Wanyama mnaowasikia usiku wanaishi huko.

**JUMANNE**; Tutakwenda mchana bibi halafu usihofu tutakuwa watu wengi.

Jumanne alijibaraguza kuongea kwa kujiamini ili aruhusiwe kwenda bwawani kujifunza kuvua samaki wakati nyuma ya pazia moyo ulimwenda mbio kwa hofu. Alitamani aende ili amthibitishie Mwanakheri kuwa yeye ni kijana jasiri. Alikumbuka mazungumzo yao muda wa kuagana;

**JUMANNE**; Kesho nakwenda Nanganyamwa kuvua samaki. Tutakwenda na washikaji zetu.

**MWANAKHERI**; toba! Utaweza kweli?

**JUMANNE**; Kwanini nisiweze? Naweza!!!

**MWANAKHERI**; Naomba usiende..!

**JUMANNE**; Ondoa shaka bibie, mimi sio goigoi.

*Sasa hasipokwenda! Aliwaza;*

**JUMANNE**; "Mwana atanidharau na kuniona goigoi."

Bibi alijua imetumika nguvu kubwa kuwashawishi vijana hao wamjini ili waweze kukubali kwenda bwawani kuvua. Isingelikuwa rahisi kufuta wazo hilo akilini mwao. Kwa kuwa hakupenda kuwafadhaisha wajukuu zake. Alisema;

**BIBI**; Haya nendeni lakini muwe makini na waangalifu. Mkifika msituni mjihadhari kucheka ovyo hata kama mtaona vibweka na vichekesho, jitahidini msicheke. Ugomvi na kisirani havifai msituni. Kama kuna mtu ana fundo alilolitunza moyoni na kupanga kwenda kuonesha jeuri huko ni bora msiende.

**CATHBET**; Mimi nashauri tusiende.

**JUMANNE**; Kipenzi changu, naomba uturuhusu twende tukajifunze. Baba atafurahi sana nikienda kumsimulia kuwa nilifika hadi msituni. Naomba useme umekubali.
**BIBI**; "*Alitabasamu"* nimeshawaruhusu ila chukueni tahadhari kama nilivyokwisha washauri.
**WOTE**; Asante bibi.
**CATHBET**; "Alimshika mkono."
**BIBI**; Msijali wajukuu zangu. Chakula kipo ndani karibu na jiko. *"Jiko la kuni lililotengwa mafiga ukumbini."*

## Msituni

Sauti za ndege na wadudu zilisikika na kutengeneza mpangilio murua wa sauti kama vile mtu anapiga marimba.

Msituni waliambatana vijana saba nao ni; Jumanne, Cathbet, Zuberi, John, Kinandi, Kaisi, na Mambo. Vijana wote walikuwa wenye rika moja isipokuwa Kaisi na Mambo, wao walikuwa na umri mkubwa zaidi. Uwepo wa Mambo na Kaisi katika safari hiyo, ndicho kilichompa afueni bibi yake Jumanne hadi kukubali kutoa ruhusa.

Kabla ya kuingia kwenye msitu mnene walikiona kibanda kilichopauliwa kwa kutumia nyasi na mianzi michache halafu sehemu ya chini ilikuwa wazi pasi na kuta. Uwanja ulikuwa mkubwa na msafi ndipo Mambo alipowaambia Jumanne na Cathbet wakae juu ya gogo ili wasubiri amalize kukamilisha shughuli fulani. Walistaajabu walipomuona anaokota ufagio na kuanza kufagia chini ya

 © 2021

kibanda hicho lakini hawakutia neno. Vijana wengine waliosalia walitumia muda huo kuweka chambo vizuri na kurekebisha mishipi. Baada ya mambo kumaliza kufanya usafi kibandani hapo, waliondoka na kuendelea na safari.

*Cathbet aliuliza kwa kudadisi;*
**CATHBET**; Mwenyewe yuko wapi?
**MAMBO**; Nani?
**CATHBET**; Mwenye eneo hili? *"Alionesha wakiwa mwisho wa uwanja wanaondoka"*
**MAMBO**; Hayupo! Ni mila zetu.
**CATHBET**; Sasa mbona haujaniambia? Tungefagia pote pale chap chap!
*Wote walicheka.*
Waliendelea kutokomea msituni huku sauti za ndege na wadudu zikiongezeka. Ingawa ilikuwa siku ya jua lakini lilionekana kupotea na joto kupungua kila walipozidi kwenda mbele. Majani makavu yaliyodondoka njiani yalizidi kuleta kelele na ghafla walisikia;

**SAUTI**; Kwi!........kwi!…….kwi!

*Walitazama juu ya mti na kuwaona ngedere. Jumanne alisita kidogo kuendelea kutembea;*

**KAISI**; Jumanne twende, tumbili tu hao!
**JUMANNE**; *"Alimgeukia Kaisi na kutabasamu bila kuongea chochote."*
Ngedere waliendelea kurukia mti moja baada ya mwingine kama vile wapo safari moja na wao. Mwishowe walianza

kushuka chini mbele yao na kuanza kutembea kwa miguu miwili kama binadamu. Hawakuishia hapo bali walianza kucheza kwa kuruka mbele mmoja mmoja na kuanza kujikuna mara shingoni, mara sirini, mara wanasaidiana kukunana ilimradi karaha tupu.

Vijana wote walikuwa kimya kana kwamba hawawaoni ngedere hao. Jumanne na Cathbet walikumbuka maneno ya bibi yao kuhusu vituko vya msituni pindi aliposisitiza kuacha kucheka vihoja vya msitu. Pia waliambiwa siku waliyopanga kwenda kuvua samaki kwenye bwawa la msituni;

**MAMBO**; Ninyi mmezoea kucheza kwenye mto huu mdogo au Mto Mbwemkuru tulikokwenda juzi. Ingawa ule ni mto mkubwa lakini hauna samaki wengi na wala mazingira yake hayavutii. Ninyi kunawafaa Nanganyamwa ila kunatisha na hutakiwi kucheka huonapo vituko vyovyote.

Mambo aliongea maneno hayo walipokuwa wanafua nguo kwenye mto mdogo wenye maji yenye rangi ya hudhurungi.

Jumanne na Cathbet walipendwa sana na Wanakijiji sababu ya tabia yao ya ucheshi, sio jeuri na walimheshimu kila mtu tofauti na walivyodhani walipowaona kwa mara ya kwanza.

 © 2021

*Jumanne alianza kukumbuka siku waliyoomba kupelekwa bwawani*;

**JUMANNE**; Hayo ndiyo maneno. Tupeleke huko kaka mkubwa! Hilo litakuwa bonge moja la 'picnic'.

**CATHBET**; Umenena *poa mwanangu!* Hapo ndiyo penyewe.

*Waliacha kufua nguo na kusimama wima kuonesha msisitizo wa tamaa yao juu ya safari hiyo wasiyoijua.*

**MAMBO**; Ndoano inabidi tupate mpya zile zinazingua.

**JUMANNE**; Mashhofu! Jamaa atarekebisha. *"Alimuelekezeaa kidole Cathbet."*

**MAMBO**; Basi poa. Kesho kutwa kama hali ya hewa itakuwa shwari tutakwenda sababu huko ikinyesha mvua kunakuwa hakufai.

*Ghafla kuna kitu kilifunga breki miguuni mwao na wote walishtuka;*

**KAISI**; Kumbe **nangondingo** nilijua nyoka.

*Kabla hawajakaa sawa ghafla mijusi wengine wakubwa wawili wakakatiza mbele yao. Ngedere walirukia kwenye mti na kutawanyika.*

**CATHBET**; Mmh!

**KAISI**; Hawadhuru hao ni mijusi sio nyoka. Maisha yao ni kuwinda wadudu hivyo sisi tumeharibu pozi lao.

Kuna ndege wawili walikuwa wanawazonga kwa kuwarukia na kutue vichwani, mara kwenye nguo, mara mabegani, mara juu ya mti sasa pakawa juu… chini…. Juu…chini harubu moja kwa moja.

 © 2021

*Jumanne alivuta fulana yake kimya kimya na kufunika kichwa kuzuia masikio yasidhurike kutokana na ukorofi wa ndege hao wadogo. Zuberi alipoona vile aliangua Kicheko.*
**ZUBERI**; Sasa Jumanne unaweka hivyo nguo yako unaogopa wataingia masikioni? *"Jumanne hakujibu."*

## Kuvunja miiko ya msitu

Vijana wote waligeuka nyuma kuangalia alichofanya Jumanne na kupelekea kuwa kichekesho. Kwenye msafara huo, Jumanne alikuwa wa pili kutoka nyuma akifuatwa na Zuberi aliyenyuma zaidi. Jumanne aliamua kukaa katikati ili kumkwepa Zuberi. Matokeo yake Zuberi alizidisha Kicheko na kuinama chini akishikilia magoti lengo lake lilikuwa kumfedhehesha mtoto wa mjini.

Karibu na tukio hilo kulikuwa na njia panda. Baada ya Zuberi kuridhika na furaha iliyosababisha kicheko aliinuka na kujikuta yupo peke yake. Wenzake walishaondoka ingawa aliwasikia kwa mbele wakiliza majani kwa nyayo. Aliendelea kucheka angali anatembea kuwafuata na kujikuta hawafikii. Kelele za majani ziliendelea kusikika kumbe walikuwa wanapita njia mbili tofauti zenye mwelekeo sawa. Zote zilikuwa nyembamba na zenye miti iliyochipua majani mengi hivyo kuwa kikwazo cha kuona upande wa pili. Pia majani makavu yaliyopukutishwa na miti hiyo yalimzuia Zuberi kugundua muelekeo kwa kuangalia nyayo.

**ZUBERI**; Mmh! Wako wapi hawa? Nikiwaita nitavunja masharti ya msitu, sasa chakufanya; ngoja niwakimbilie tu. *“Aliongea peke yake akipaza sauti kana kwamba alikuwa anajadiliana jambo hilo na mtu mwingine na kuanza kukimbia.”*

Alikimbia kwenda mbele bila mafanikio na punde aliacha mbio na kusimama akihema ovyo na kujiuliza;

**ZUBERI**; Mbona silikuti daraja au nimepotea? Ngoja nirudi nyuma labda walijificha mahali ili wanikomeshe.

Alirudi tena nyuma alikotoka akitimua mbio lakini ola! Palikuwa patupu. Woga ulianza kumuingia na kuamua kupaza sauti kuwaita wenzake. Aliwasikia wanaitika upande uleule alikotoka muda si mrefu na kuanza tena kukimbia kuelekea huko. Lakini alipofika huko na kuita tena, alisikia wanaitika kulekule alikotoka! Aliamua kutimua mbio kwa spidi ya duma kama vile yupo kwenye mashindano ya riadha ili awafichue wenzake aliohisi wanamghilibu ingawa hakukuwa na mtu pia. Alitupia jicho kila mahali na kuambulia kuona miti mikubwa ikizunguka kama yumo kwenye gari inayosafiri kwa mwendokasi.

**ZUBERI**; Hawa wananichezea mchezo ngoja nirudi zangu nyumbani.

 © 2021

## DARAJA LA MTI MMOJA

Jumanne na wenzake watano waliendelea na safari hadi walipofika darajani kwenye kivuko cha gogo moja. Daraja ambalo watu huvuka kwa kupishanisha mguu mmoja mmoja hadi ng'ambo. Kwa kuwa walitakiwa kuvuka moja baada ya mwingine, ndipo walipojigundua wapo sita badala ya saba kwavile Zuberi alikosekana.



**JUMANNE**; Zuberi yuko wapi?

Wenyeji walipigiana ukope kabla ya kumjibu. Sababu walishagundua kutoweka kwake muda mfupi uliopita pale waliposikia sauti yake kwa mbali ikiwaita kwa nyuma, "uuuuuu!" Ila waliogopa kumsaidia kuitika kwa kuwa waliogopa kuvunja masharti ya msitu ambapo ingepelekea wote kupotea. Ndipo walipoamua kumwacha apambane na hali yake na kama kupotea, apotee peke yake. Hawakuwa na shaka kuhusu usalama wake sababu Zuberi alikuwa mwenyeji hivyo ni rahisi kwake kurudi nyumbani pindi atakapomaliza kutumikia adhabu yake.

 © 2021

**JOHN**; Karudi nyumbani huyo.

**MAMBO**; Ndoano yake alibeba mwenyewe?

**JOHN**; Ndiyo lakini chambo hii hapa! “Alionesha”

**MAMBO**; Labda kabadilisha safari na kuamua kwenda Mtonyange maana nako kuna samaki wengi. Ingawa sasa hivi maji ni mengi sababu ya mvua zilizonyesha *kati* pale. Twendeni tukafike.

Hawakukawia kufika waendako. Cathbet alizongwa na mawazo yaliyojaa maswali lakini aliogopa kuuliza. Bwawa lilikuwa kubwa na upande mmoja ulikuwa na tope, maji kidogo, na magugu maji mengi wakati upande mwingine ulikuwa na maji angavu ambayo ndiyo waliyoyakusudia kwenda kuvua samaki.

Hivyo iliwalazimu kuvuka toka upande wa kwanza wenye tope hadi upande wa pili wenye maji angavu. Ili waweze kuvua vizuri iliwapasa wapande juu ya mizizi ya mti mkubwa uliomea kwenye maji na kutengeneza bembea. Kwahiyo Jumanne na Cathbet walielekezwa na wenyeji wao jinsi ya kukaa ili wasianguke na kutumbukia bwawani.

Vichekesho na vitisho viliendelea. Bwawa lilisheheni samaki sambamba na wanyama kama vile viboko, na mamba. Wadudu wenye muonekano tofauti tofauti waliibuka na kuzama kwenye maji kana kwamba wapo kwenye ‘kwaito’. Vipepeo, panzi, mbu, usubi na mbung’o

 © 2021

hawakucheza mbali nao. Wakati angani kulikuwa na makundi makubwa ya ndege na nyuki waliokuwa wanatengeneza duara na kutawanyika mfululizo kama wapo kwenye maadhimisho ya siku ya utalii.

Taharuki ilitawala pale ndoano ya Jumanne ilipogoma kuibuka kutokana na uzito wa kitu kilichomeza chambo. Bila kujua ni samaki, nyoka, au kitu kingine, Jumanne alijitahidi kuongeza nguvu kuinua ndoano yake lakini alishindwa na kuambua kuteleza na kuning'inia mtini baada ya kudaka tawi kwa mkono mmoja na mwingine kuendelea kushikilia ndoano. Kaisi alikuwa amekaa karibu nae alimrukia na kumdaka almanusura wazame wote majini. Wenzao walisogea na kuwaokoa. Kumbe alinaswa kambare aliyepea na kilichostaajabisha zaidi ni pale samaki huyo alipoungana na samaki wengine walioendelea kung'ata mkia hata baada ya kambare mzee kufikia ubigoubigo wa maji.

Jumanne na wenzake walifurahia masaibu hayo kisha waliendelea kuvua hadi walipoona mwanga unazidi kufifia na kutambua kuwa jua litakuwa limeshatua Magharibi. Ni nadra sana kwa eneo hilo kuliona jua kutokana na giza linalosababishwa na msitu mnene wa mitomondo.

Kila mmoja aliwaweka samaki wake kwenye mtungo kisha kuanza safari ya kurudi nyumbani. Jumanne ndiye aliyeongoza kupata samaki wengi kuliko wenzake na

katika msafara yeye ndiye mwanagenzi wa uvuvi ukilinganisha na wengine.

Punde walifika kwenye daraja la mti mmoja na kama kawaida walianza kuvuka mtu moja moja. Jumanne alipofika katikati ya daraja samaki walianza kupupa na kumfanya abadili mkono ili ashike vizuri kwa kutumia mkono wa kuume na baada ya kufanya hivyo mtungo wa samaki ulifunguka. Katika kubabaika ili kujinusuru kutumbuki mtoni, samaki wote waliponyoka na kumwagika kisha kubakia mtupu! Kambare mkubwa ndiye aliyekuwa wa kwanza kutoroka sababu bado alikuwa yu hai. Ingawa baadhi yao walishakufa, haikusaidia kuokoa zahama hiyo kwa sababu samaki hao walipotua majini walielea na kuzolewa na maji yaliyopita kwa kasi kuelekea bondeni.

**MAMBO**; Pole sana bwana mdogo, usilie. Twende nyumbani angalau samaki wa ndugu yako wamebaki. Ni bahati mbaya imetokea kwako.

**JUMANNE**; ‘Ok’ poa! Daah! Samaki wangu.

**CATHBET**; Twende Juma usilalamike sana si unajua tena? Twe’nzetu! “Alimshika mkono na kumtanguliza mbele yake.”

Vijana wote walimpa pole Jumanne na kumchangia samaki. Alifurahi kidogo ingawa alimfikiria sana kambare wake wa kihistoria ambaye alipanga kupiga nae picha na

wakirudi Dar-es-salaam aiweke Facebook au WhatsApp hivyo alijikongoja na kusema;

**JUMANNE**; Asanteni sana! Hapa nimefarijika sababu mpenzi wangu Mama Liganga atapokea kitoweo kwa ajili ya mlo wa leo.

Wote walicheka. Walipenda namna anavyotumia utani katika mazungumzo yake. Walimuita, “Mzee wa madongo” sababu aliweza kumwambia ukweli mtu aliyekosea kwa kutumia maneno ya utani bila kumweka kwenye tahayuri.

Waliendelea na safari ya kurudi nyumbani na ghafla waliona kitu kimeegemea kwenye mti;

**JOHN**; Yule sio mtu?

**KAISI**; Mbona kama Zuberi? Naona nguo kama……!

**KINANDI**; Ndiye huyo huyo….!

Muda wote Kinandi si mzungumzaji kazi yake ni kutabasamu na kushughulika bila kutia neno.

Mambo alisogea karibu ya mti huo kisha kumwamsha Zuberi aliyezama kwenye lindi la usingizi na kulala fofofo.

**MAMBO**; We! We! We! Zuberi!

**ZUBERI**; M…..m….m! *“Alifumbua macho na kuinuka kwa haraka akijikung’uta mwili kana kwamba kagandwa na wadudu na kusema,*” …..twendeni…..! Chambo yangu ipo

wapi? Shembea? *'alijipapasa kiunoni"* A…a..a..! samaki? Sasa ….sa..mi…mimi…mbona sielewi?

**MAMBO**; Twende huku….!. "Alimsukumizia kwenye njia ya kuelekea nyumbani."

Kidogo kidogo Zuberi alianza kurudisha kumbukumbu. Alikumbuka, alikimbia huku na kule hadi baadaye alisikia anaitwa jina lake kila upande kwa sauti yenye kupokezana iliyoambatana na mwangwi. Ilisikika;

**SAUTI**; "Zu…be….riiiiii! Zu…be….riiiiii!"

Alipatwa na kizunguzungu na kuamua kuegemea mti ili apumzike kidogo kurudisha nguvu ili aweze kurudi nyumbani na ndipo mahali walipomkuta wenzake.

**ZUBERI**; "Aliwaza kimya kimya akiwa anaendelea kutembea" ……njia hii ilivyokuwa kubwa na kutumiwa na watu wengi ina maana hakuniona mtu yeyote hadi nilipokutwa na wenzangu tena pale pale karibu kabisa na waliponiacha?

Zuberi alishtuliwa kutoka mawazoni pale Mambo alipompa samaki wawili kwa ajili ya kitoweo cha siku hiyo. Alimshukuru na punde walifika kijijini. Mambo akiwa ndiye Mkuu wa msafara, aliwaonya vijana kutosimulia matukio yaliyojitokeza msituni na ibaki kuwa siri ya safari. Walikubaliana kutunza siri na kila mmoja alielekea nyumbani kwake.

**Nyumbani;**

Bibi yake Jumanne alifurahi sana alipowaona wajukuu zake wamerejea salama salimini tena wakiwa wamepata samaki.

**BIBI**; Poleni sana! “Aliwapokea.”

**WOTE**; Asante

**BIBI**; Waume zangu leo mmetoka kuhemea. Ndoa mali! Maana tangu Mzee Kinje afariki, sijawahi kupata huduma hii. Sasa leo……! “Alifunga vizuri ashukuri halafu aliinua vidole juu kama shambenga.”

Wote walicheka na kumshukuru kwa sifa alizowamwagia sababu ziliweza kuwavimbisha vichwa na Jumanne alikumbuka kambare wake na kujisemea;

**JUMANNE**; Angelikuwepo kambare mkubwa, leo ningeliosha sana kwa bibi. Basi tena kisicho riziki…….!

 © 2021

# MIZIMU

## SIMBA MWENYE MJI 'NAKANJI'

Siku iliyofuata; baada ya kupata staftahi ya mwiku wa wali kwa samaki wote wakiwa ukumbini, walianza kupiga porojo. Jumanne na Cathbet walikaa juu ya kitanda kidogo cha kamba, miguu wakiburuza chini wakati bibi yao alikaa kwenye mkeka. Ndani ya gumzo, Jumanne alichomekea udadisi wake kuhusu kibanda walichokiona njiani walipokuwa wanaelekea bwawani. Pia alihitaji ufafanuzi juu ya mila iliyopelekea Mambo kufanya usafi kwenye uwanja wa kibanda hicho. Alianza kwa kusema;

**JUMANNE**; Jana asubuhi Mambo alifagia kwenye kibanda fulani chini ya miti lakini hakuwepo mwenyewe.
**BIBI**; Angalikuwepo mwenyewe ninyi msingaliweza kupita.
**CATHBET**; Anatisha sana au anazuia watu kupita?
**JUMANNE**; Ni kichaa? Sasa kwanini kamfagilia na jitu lenyewe ni likorofi au ni ndugu yake?
**BIBI**; Sio mtu. "Alijibu akicheka."
**CATHBET**; Eeh! "Aliinuka na kushika miguu" …umesemaa?
**BIBI**; Sio binadamu bali ni simba…!
**WOTE**; Eeh! Mama yangu…..!

Walikurupuka na kukaa vizuri wakitazamana mikono yao ilikosa utulivu kabisa! Na kujikuta wakijishika mara puani,

mara mashavuni ilimradi tafrani. Kisha walipata maneno baada ya kigugumizi kutoweka;

**JUMANNE**; Unajua 'best' jana tulichezea hatari?

**CATHBET**; Mimi siendi tena.

**BIBI**; Hayo ndiyo maisha yetu wajukuu zangu.

**JUMANNE**; Nieleze kuna uhusiano gani wa simba na watu kufagia….yaani ……sijaelewa. Au bibi unataka uturekebishe tusiende tena? Shemeji yako umeshamsikia alivyotoa ya moyoni na mimi barabarani tu yaani mulemule!

**BIBI**; Hapana wanangu sio kama ninawatishia. Wenzenu hawakuwaambia ukweli sababu walijua safari ingeliishia hapo hapo. Anaitwa NAKANJI ni simba mzee mwenye mji wanasema, "hapo zamani za kale alikuwepo mtu maarufu halafu aligeuka simba baada ya kufariki."

**CATHBET**; Eeh! Sasa …..Mambo ni familia yake?

**BIBI**; Sio Mambo pekee yake bali sisi sote tunatakiwa kufagia. Tofauti ya simba huyo na simba wengine ni kuwa Nakanji hadhuru watu bali hulinda na kufukuza simba wala watu.

**JUMANNE**; Natamani nimuone ni…….!

**BIBI**; Wee, ishia hapo hapo! *"Bibi aliweka ukili pembeni na kusema,"* ……temea mate chini.

*Jumanne ni hodari wa kufuata maelekezo hivyo alitema mate.*

**JUMANNE**; Tuuuw! Vipi tena? Umesema yeye oya! Oya! Yaani kama mbuzi tu au?

*Walicheka!*

**BIBI**; Subiri nikupe kisa cha marehemu shemeji yangu ambaye alifanana mawazo kama yako. Shemeji alikuwa Mwanajeshi huko Ngerengere mkoani Morogogo hivyo waliishi huko huko kambini na kuja kututembelea nyakati za likizo. Siku moja nae alisema kama wewe, *"natamani kumuona simba huyo na ikiwezekana nipigwe nae picha."* Dada alimwambia, '*usikufuru mume wangu!'* lakini yeye aliendelea kukaidi. Enzi hizo Nilikuwa kigoli mwali hivyo nilikuwa naelewa kila kitu kwa usahihi na kuwa na kumbukumbu navyo. Aliendelea kusisitiza kuwa hamuogopi simba sababu kwao Arusha hawawezi kuoa hadi waue simba saba. Kila tulivyojaribu kumzuia kuongea maneno ya shombo juu ya Nakanji, alisimamia msimamo wake na alikataa katakata kukaa kimya.

"Kabla ya likizo kwisha mvua kubwa ilinyesha. Walikuwa wamekamata shamba kufuata mlizamu wa maji ya mto Mbwemkuru. Lengo lao lilikuwa wapande mpunga. Baada ya mvua kuacha kunyesha na kubakia rasharasha, alikwenda kuona shamba ili kujua kama kweli udongo ulitota maji kiasi cha kufaa kusia mbegu."

‘Shambani alikwenda peke yake sababu hayupo aliyelandana mshawasha wa kulima kama yeye. Watu wengi walisema, “analimia nemsi” kwa sababu haikuwa ajira yake ya maisha. Laiti ingelikuwa maisha yake ni yale ya jembe na mtu yamkini angeliweza kuichukia mvua.”

‘Kuthibitisha mvua iliyonyesha ilikuwa kubwa, wadudu wa aina mbalimbali walijaa angani wakiwemo kumbikumbi. Kelele za vyura nazo zilikaribia kutoboa ngoma ya sikio. Hakujali lolote, aliendelea kubonyeza ardhi kwa kutumia kidole na mara nyingine vijiti na kushtuka jua limezama Magharibi. Giza lilichukua nafasi taratibu na kuanza kuchwa. Alizungumza peke yake,”

**BABU**; Ngoja nirudi nyumbani jua limekuchwa. Kesho nitakuja kupanda mapema. Mama Grace atanikuta nimeshafika palee! Pale pote patakuwa tayari nimeshapanda mpunga. “Alirushia vipande vya udogo kuonesha maeneo.”

## Usiombe ya kukute

*“Kijiji kinaonekana kilee!*

Ghafla alisikia pa..pa..paaaaw! pa…pa..paaaaw! Sauti kama mtu anagonga debe. Ilikuwa ni ngurumo ya simba aliye karibu. Mzee alisimama na kuwaza kujificha au kurudi nyuma. Alikumbuka hakuna kijiji maeneo ya karibu na shamba lake hadi ng’ambo ya mto ambao umeshaanza kutiririsha maji ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha

maeneo ya milimani. Mbele yake ndiko ngurumo ilikosikika. Alichagua kujificha katika kichaka kilicho karibu na kichuguu. “

**BABU**; Mmh! Au ndiyo simba wao wa makaratasi sijui mdoli? Ebu mimi niondoke zangu. Kama haumi sasa ninaogopa nini?

“Jamaa alijitoma njiani ili kuendelea na safari. Ile kutokeza tu njiani! Alig’atwa na mdudu na kumsababishia maumivu makali ingawa alishindwa kujua ni mdudu gani. Wadudu wengi walitambaa karibu na vichuguu kuwinda kumbikumbi. Hata wanyama kama mbweha, vicheche, na fisi hawakucheza mbali na maeneo hayo.”

**BABU**; Mama wee! *“Alilia kwa kupanza sauti na kupangusa kilichomuuma kwa kiganja cha mkono na ndipo kilipomng’ata tena kidoleni.”*

‘Alikaa chini kusikilizia maumivu na kusahau kama kuna habari za ngurumo za simba.”

**BABU**; Ubaya wa kutembea bila kuvaa buti matokeo yake ndiyo haya. “Alijisemea.”

‘Alisikia kwa…..kwa…..kwa kama vile kuna watu wanakimbia mchakamchaka kuelekea alipo. Muda huo tayari nuru ya jua ilishapotea na mwezi kuandama ila ulikuwa na tanga la mvua hivyo kutoa mwanga hafifu.

 © 2021

Aliinuka na kusimama wima. Aliona mwanga kama tochi mbili zinamfuata,”

**BABU**; Tochi? Sasa huyu ndiye nani tena?

**BIBI**; ‘Aliinama ili kupachika vidole kwenye kandambili. La haula! Alipoinuka tu, alikutana uso kwa uso na kitu kilichoshiba vizuri kabisa na kina nyusi zenye kukaribia kufunika sura yote. Alikuwa simba mwenye mji. Kabla shemeji hajapata wazo, simba alianza kujinyoosha akiwa amepanua midomo mithili ya mwayo. Meno marefu yaliyoshika rangi ya njano na kutoa harufu mbaya ya mizoga, yalizidi kuvuruga akili ya Mwana-Anga huyo. Alijikuta amesahau masuala ya Nakanji, simba mwenye mji nakuwaza jinsi yakujiokoa.”

‘Alipogeuka! Alikula mweleka na kudondoka chini pwaaa! Alijaribu kujiinua lakini alidondoka tena. Alijikongoja na kufaulu kuinuka tena na mara hii alipotea njia na kujikuta ameingia uvunguni mwa simba. Simba aliacha kupiga mwayo ndipo shemeji aliposhtuka kuwa yupo hatarini zaidi na kuanza kurudi nyuma taratibu. Bahati haikuwa upande wake, alitereza na kudondoka tena. Alijiburuza na kuanza kukimbia miguu minne kama nyani vidole vya mikono viliburuza chini bila kuangalia mbele wala juu na alikwenda kuparamia kichuguu. Kwa kuwa udongo ulilowana na maji ya mvua alitereza na kuporomoka hadi chini pwaa! Kama furushi. Alienea mabawa ya kumbikumbi mwili mzima……! Kishindo kiliwashtua

wanyama waliokuwa mawindoni kama vile fisi, mbweha, vicheche, nguchiro, panya walikimbia na simba pia alikimbia. Bwana yule alipoteza fahamu pale pale!”

‘Nyumbani wasiwasi ulianza kutuingia, kulikoni aliyekwenda shambani tangu Alasiri harudi na Nakanji amenguruma maeneo ya huko huko alikoelekea yeye?”

‘Walikwenda wazee watatu na vijana wawili wakiwa wamewasha mwenge na kubeba panga na rungu. Walimkuta shemeji akiwa hajitambui. Kachafuka mwili mzima, hatamaniki! Kilichosaidia ni michirizi ya uterezi iliyoonesha muelekeo kutoka njiani. Alipozinduliwa kwa kutumia majani ya miti walirudi nae nyumbani na kesho yake waliondoka kurudi kwao Morogoro badala ya kwenda shambani kupanda.”

*Cathbet na Jumanne walitazamana;*

**JUMANNE**; Nipeleke nje nikakojoe.

**CATHBET**; Nani? Mwambie bibi au kama vipi kakojoe kwenye kopo. Mimi nilishaliingiza ndani nilipoona habari hii siielewi.

**BIBI**; Khaa! Na jua lote hili? Msiogope wajukuu zangu. Nakanji anajua ninyi ni watoto hivyo hawezi kuwatishia.

***

Ilipofika mchana Jumanne alimtafuta Mwanakheri na kumsimulia mambo yote yaliyotokea katika safari yao.

 © 2021

Mwanakheri alimtafsiria maana ya mikasa iliyotokea kuwa; sababu ya kukatika mtungo wa samaki ni kuwa bibi yake hakuridhika aende bwawani na Zuberi alipotea sababu alicheka vihoja vya msitu.

## KIMOMBO

Ndani ya msitu huo wakutisha, kulikuwa na bwawa lenye viboko wenye uwezo wakuwasiliana na binadamu. Kiongozi wa viboko hao aliitwa Kimombo. Hivyo kabla ya safari ya kurudi Dar-es-salaam, Jumanne na Cathbet walipanga kwenda kuitembelea familia ya Kimombo. Walipelekwa na msimamizi wa kimila wa msitu huo aliyetambulika kwa jina la Bwana Mnajimu.

Kimombo aliwaonesha wake zake, watoto na ndugu wengine wote kwa zamu. Safari hii waliokwenda msituni ni; Cathbet, Jumanne, Mwanakheri, Kaisi, Hidaya, Mambo, John na Mnajimu mwenyewe.

*Mnajimu husema "Kimombo tunakuomba utuoneshe watoto wako!"*

Watoto wa kiboko waliibuka na kurusha maji juu.

"Tayari inatosha sasa tuoneshe wazee" nao hufanya hivyo hivyo hadi rika zote zilizotajwa zilipoisha kisha kumuomba ajitokeze mwenyewe. Naye pia hufanya hivyo! Hutoka nje

 © 2021

na kurudi ndani ya maji aliporuhusiwa kufanya hivyo. Kimombo ni kiboko mkubwa sana

Walirudi nyumbani kwa furaha na kuagana kwa ahadi ya kutembelea tena likizo itayofuata. Walipeana zawadi za kumbukumbu pamoja na namba za simu. Mwanakheri aliugua homa ya tumbo siku ambayo Jumanne alifanya safari ya kwenda kwao Dar-es-salaam. Jumanne alimshauri aende zahanati ili apate vipimo pamoja na matibabu. Kwa kuwa ili wafike stendi walitakiwa kupita kijiji ambacho huduma ya afya ilipatikana, waliamua kuambatana nae hadi zahanati. Walimuacha Zahanati akihudumiwa halafu wao waliendelea na safari.

Jumanne na Cathbet walimshukuru sana bibi yao na kupanda basi kurudi mjini. Njiani waliyapita malori mengi yaliyobeba jasi inayochimbwa kandokando mwa msitu wa hifadhi kisha kusombwa kupelekwa viwandani jijini Dar-es-salaam. Basi likiwa barabarani linaendelea kukata upepo, cathbet alikumbuka maagano yao na hali ya kiafya ya Mwanakheri.

**CATHBET**; Hivi itakuaje endapo Mwanakheri akibainika ni mjamzito?

Aliondolewa mawazoni pale Kondakta alipowafikia kukagua tiketi zao.

***

*Nyumbani kwa Wazazi wa Jumanne;*

Walipokelewa na Baba Jumanne katika kituo cha mabasi ya kwenda mikoani cha Ubungo. Walizungumza mengi na

walipofika nyumbani wote walifurahi na kutamani wasimuliwe michapo ya kijijini.

*Chumbani usiku;*

**BABA JUMANNE**; Wiki ijayo nitaanza likizo, nimepanga kwenda kijijini kwa Mama'ngu.

**MAMA JUMANNE**; Kunani tena jamani? Mwanao ndiyo kwanzaa! Kafika leo au kaleta maagizo ya kuwa unaitwa?

**BABA JUMANNE**; Hapana, sijaitwa ni likizo. Unataka niendelee kukaa hapa hapa sio?

**MAMA JUMANNE**; Ukienda huko kijijini nami naomba uniandalie fungu langu ili niende nikamtembelee shangazi yangu Kondoa. Ukirudi nami nitarudi. *"Alijibu kwa hasira sababu alizoea likizo ya mumewe waliitumia kutalii kwenye vivutio mbalimbali na starehe."*

**BABA JUMANNE**; Hapana nikirudi wewe endelea kukaa huko huko! Wewe kama ulitaka kwenda nyumbani kwenu ungesema na kamwe nisingekuzuia. Halafu kama tatizo ni kubakia peke yako hapa bila uwepo wangu, kwanini usiseme twende sote tukamuone Bi. Mkubwa? Sasa mimi nitakwenda na sikupi fungu lolote la safari yako. Ukijifanya unayo nauli, nenda na usirudi milele! Kakae huko huko na ndugu zako.

Baada ya kuzungumza hayo alitoka na kwenda kukaa sebuleni. Alimimina mvinyo kwenye bilauri kubwa maalum

 © 2021

kwa ajili yake na kuanza kugida akisindikiza na misonyo “fyoooo! fyoooo!” na kuendelea kunywa taratibu dengelua ya mashineni. Alikumbuka nyumba ya mama’ke na maisha kwa ujumla kama alivyoelezwa na mwanae Jumanne.

Hivyo alifikiria kwenda kumjengea nyumba nzuri na kukaa nae kwa muda kwa ajili ya kujipatia baraka toka kwake. **BABA JUMANNE**; Mama ni mama tu. “Aliongea peke yake.”

*Mama Jumanne alijisogeza kwa upole;*

**MAMA JUMANNE**; Samahani mume wangu sitarudia tena kukujibu vibaya. Wewe utakwenda na utanikuta hapa hapa! Naomba unisamehe na usinifikirie vibaya. Pole sana mahabubu. Inuka twende chumbani tukalale. “Alimshika mkono na kumwinua.”

Walikumbatiana…….!

MWISHO.

 © 2021

**Nangondingo**: Mjusi mkubwa mwenye kichwa chenye rangi ya bluu.

 © 2021